

FASIHI SIMULIZI KATIKA MUKTADHA WA UANUWAI WA KIMAWASILIANO NCHINI
KENYA

Collins Kenga Mumbo
Chuo Kikuu cha Moi

Ikisiri

Katika jamii ambazo zimetegemea zaidi mbinu za kimasimulizi kuliko mbinu za kimaandishi kuwasilisha maoni, falsafa zao na utamaduni wa jamii zao, fasihi simulizi imechukua nafasi muhimu. Kwa muda mrefu, jamii nyingi nchini Kenya, fasihi simulizi imekuwa njia muhimu ya kueneza na kuwasiliza mawazo, maarifa na historia. Katika makala hii ninadadisi jinsi tanzu mbalimbali za fasihi simulizi zinavyoweza kuendelezwa katika enzi hii ya uanuwai wa njia za mawasiliano; ni vipi utendaji na vipengele vingine vya fasihi simulizi vinarekodiwa, kukusanywa, kuhifadhiwa na kusambazwa kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano ukiwemo mfumo wa digitali. Makala hii imejikita katika aina mbili za fasihi simulizi; kwanza ile fasihi simulizi ambayo imekuwepo tangu jadi; hadithi simulizi, mashairi simulizi, majigambo, matambiko, maigizo, vitendawili, methali na misemo, na ngoma inahitaji kuhifadhiwa na kuimarishwa. Pili, ni ile aina ya fasihi simulizi inayoumbwa na kuzalishwa kutokana na teknolojia ya kisasa pamoja na njia za kisasa za mawasiliano kwa mfano vibonzo hai na vikaragosi. Pia, uzalishaji au ubunaji wa maumbo mapya utashughulikiwa. Uchunguzi huu vile vile utaangazia mchango wa taaluma zinazohusiana na fasihi simulizi ikiwa ni pamoja na isimujamii, sanaa na sanaa za maonyesho, anthropolojia, historia, dini na utamaduni katika muktadha wa mawasiliano ya kisasa.